

**Learning by Ear 2012**

**Series: Everyone's Different - Respect for Minorities**

**Episode 9: The World of Aminata, A Widow in Senegal**

**Author: Babou Diallo**

**Editor: Friederike Müller / Yann Durand**

**Characters:**

- **Aminata, a widow (f, 25), French**  
Pronunciation: as written
- **Mamadou Dabo, a teacher (m, 35), French**  
Pronunciation (german): [Mamadù Dabò]
- **Hélène, a married woman, Aminata's neighbour (f, about 30), Wolof**  
Pronunciation (german): [E-lään]
- **Idrissa Konaté, Islamic scholar (m, 41), French**  
Pronunciation: as written
- **Aliou Fofana, sociologist (m, 37), French**  
Pronunciation (german): [Ali-u Fofanà]

**Pronunciation:** Oumar: [Umar]  
Babou Diallo: [Babu Diallo]

**INTRO:**

Karibu kwenye makala ya **Noa Bongo Jenga Maisha Yako** na katika sehemu mpya ya mfululizo wetu unaoendelea uitwao, ‘ **Kila mtu ni tofauti-Kuzingatia maslahi ya jamii za walio wachache**’. Leo hii tutazungumzia wajane barani Afrika, hasa nchini Senegal.

Wajane ni miongoni mwa makundi ya watu wachache wanaotatizika sana maishani. Nchini Senegal, sawa na maeneo mengine barani Afrika, wajane wanakabiliwa na maisha magumu. Kugharamia elimu ya watoto wao, kuhakikisha kwamba wana chakula na makazi- hazi ni baadhi tu za changamoto zinazokabiliana nao kila siku. Wakati mwingine hawasaidiwi na jamaa zao, jamaa za mume au jamii kwa ujumla. Hayo ndiyo masahibu yaliyompata Aminata, ambaye alifiliwa na mume wake miaka miwili iliyopita. Mazungumzo yake yanaonyesha jinsi maisha yalivyo magumu kwa wajane wengi nchini Senegal.

**1. ATMO: room interior**

**2. NARRATOR:**

Mwanamke anayeonekana dhaifu wa mwili, na ambaye ni mweusi amekaa kwenye kochi na simu sikioni. Macho yake ameyaelekeza kwenye televisheni. Hivyo ndivyo, Aminata anavyoanza shughuli za jioni.

Ni saa kumi na mbili jioni na kuna baridi kiasi. Aminata anaonekana kama mwanamke wa umri wa makamo. Anawalea watoto wake watatu- mabinti wawili, mmoja wa umri wa miaka 10 na mwengine wa umri wa miaka 8 na mvulana mwenye umri wa miaka 6. Aminata anawalea watoto wake yeye binafsi hapa katika eneo la Niarry Tally, ambalo lina wakazi wengi sana katika jiji la Dakar.

**3. CLIP AMINATA (French)**

*Tangu mume wangu alipofariki dunia, mimi na wanangu tumekuwa tukisimamiwa na kampuni ambayo mume wangu alikuwa akiifanyia kazi. Mimi hukabidhiwa mshahara wake wa kila mwezi kwa kuwa alifariki kabla ya kustaafu. Hizi ndizo hela zinazotukimu, nazitumia kulipia kodi ya nyumba, kodi ya maji, nguvu za umeme, na pia kuwalea watoto.*

#### 4. NARRATOR:

Mimi hupewa kiasi Yuro 115. Si kiasi kikubwa cha fedha. Hata hivyo, Aminata ana bahati kama mtende. Wajane wengine wengi wangetamani sana kupata hicho akipatacho. Si wanawake wote wanaofiwa na waume zao wanaopata usaidizi wa kifedha. Na wakipewa, mafao wapatayo barani Afrika ni kiasi kidogo sana, na hulipwa mara tatu kwa mwaka, maanake ni kati ya Yuro 50 na Yuro 70 tu.

Aminata alikuwa na raha maishani. Mumewe alijitahidi kuhakikisha kwamba Aminata aliishi maisha mazuri. Kwa mfano, alikuwa akimnunulia zawadi nzuri nzuri. Anakumbuka hali ilivyokuwa wakati huo. Aidha anakumbuka siku ambayo mumewe alitoweka: Oumar alifariki kwa ajali ya barabarani alipokuwa akirejea nyumbani kutoka kazini. Alikuwa na umri wa miaka 28. Ingawa Aminata alihuzunika sana, hakukata tamaa:

***KW begins***

#### 5. CLIP AMINATA (French)

*Ninajitahidi niwezavyo. Ninashughulikia wanangu peke yangu. Kwa sababu aliniachia watoto wachanga. Sasa nashughulika kulea watoto wangu.*

#### 6. CLIP AMINATA (French)

*Ninapokumbana na matatizo, humuomba Mungu anisaidie na anipe ukakamavu. Pia kwa kawaida mimi hutathmini mambo nijue uzuri na ubaya wake.*

***KW ends***

## 7. SENEGALESE RAP

(Note to the editor: NB - only 10 seconds, then fade under text)

## 8. NARRATOR:

Kila anapousikiliza wimbo huu wa Maxi Crazy, hupata ujasiri. Ujumbe wa mwanamuziki huyu wa Senegal, anayeimba nyimbo za kufoka foka, ni: maisha ni mapambano, na mtu hapaswi kukata tamaa. Wajane wengi wanafahamu vyema maana ya ujumbe huo. Mara nyingi wao hutelekezwa na familia za marehemu za waume zao. Hawana budi kukabiliana na dhiki za maisha ya kila siku, wanajilisha na kujivisha mavazi, wanawalea watoto wao, na kadhalika.

Katika hali kama hiyo wajane hao wanapaswa kujisimamia vyema- kama afanyavyo Aminata. Anawashauri wajane hao kuiga afanyavyo:

## 9. CLIP AMINATA (French)

*Mimi huwaambia nilivyofanya hata nikaondokana na masaibu. Wanataka kujua jinsi ninavyoweza kufanya nifanyavyo, ikiwa ninapewa msaada na mashemeji zangu. Mimi huwaambia hapana. Ninajisimamia kwa hicho kiasi kidogo cha mshahara ambacho mume wangu alituachia. Ninawakimu wanangu na kila kitu kwa hicho kipato kidogo. Hata hivyo, hutumia kiasi kidogo cha hizo hela kufanya biashara. Hutumia faida ninayopata. Sifanyi ubadhirifu kwa sababu nina watoto wachanga wanaohitaji malezi. Mimi ndiye baba na mama yao. Huu ndio ushauri ninaowapa marafiki zangu wajane. Baadhi yao hufuata ushauri wangu.*

***KW begins***

**10. NARRATOR:**

Aminata ameanzisha biashara ndogo. Pembe moja ya chumba chake cha maongezi ameifanya mahali pa kuuzia bidhaa zake, kwa sababu hana maskani ya kufanyia biashara.

**11. CLIP AMINATA (French)**

*Basi: hapa, mimi hununua viatu ambavyo huwapa wateja na kulipa kwa awamu. Aidha nina mambo mengine madogo madogo ambayo mimi hufanya kujipatia fedha: mimi huuzua aina fulani ya kalimati ziiwazo accra na pia mikate ya maji, ambayo inapendwa sana na watoto. Mwishowe, hupiga hesabu kuona faida niliyopata ili nihiifadhi.*

***KW ends***

**12. ATMO: in the courtyard of the house**

**13. NARRATOR:**

Watoto wa Aminata wanacheza kwenye ua wa nyumba pamoja na watoto wa jirani yake, Héléne. Aminata na Héléne wanaishi katika ghorofa moja. Ingawa ana umri wa miaka 30 na kitu, ameolewa na ana watoto wawili, anasema anawasikitikia kina mama wenzake wajane. Hana uwezo wa kuwafaa kwa mali, lakini hujaribu kuwapa nasaha na pia kuwasaidia vyovyote vile anavyoweza.

**14. ATMO: Atmo including the sound of *mbalax*, Senegalese music**

**15. CLIP Hélène (Wolof)**

*Nadhani ni jukumu letu kuwasaidia kina mama hawa. Laiti ningekuwa na uwezo ningewasaidia. Si wajane tu; pia tusiwapuuze wanawake ambao wametaliwiwa na waume zao.*

**16. NARRATOR:**

Siye pekee aliye na maoni hayo.

**17. ATMO: in the street**

**18. NARRATOR:**

Mamadou Dabo ni mwalimu. Anaishi katika eneo sawa na Aminata. Yeye pia anatoa wito wa kuwasaidia wajane. Anawasikitikia sana kina mama hawa.

**19. CLIP MAMADOU DABO (French)**

*Sheria inapaswa kupitishwa bungeni kushughulikia hali ya kina mama hawa, ambao mara nyingi hutelekezwa.*

**20. NARRATOR:**

Hata hivyo, si wanaume wote walio na mtazamo huo. Mara nyingi wajane hubaguliwa wakabaki wakiteseka. Baadhi ya wanaume wanaitakidi kwamba wanawake hao ndio waliowasababishia mikosi waume zao. Ndio sababu huwa vigumu kwa mjane kuolewa tena. Asilimia 95 ya wakazi wa Senegal ni Waislamu. Je unyanyapaa huo unasababishwa na Uislamu?

Idrissa Konaté ni msomi wa Kiislamu. Kulingana na maoni yake, hakuna sababu ya kumfanya mtu kupinga ndoa kama hiyo. Kuna ushahidi kwamba Mtume Muhammad- ambaye ni dira ya kuongoza Waislamu- aliwahi kumuoa mwanamke mjane.

**21. CLIP IDRISSA KONATE (French)**

*Siwezi kudai kuwa mimi ni mfuasi wa Mtume Muhammad kisha nipinge kuoja mjane. Hapana. Lakini kuna watu wanaofikiria hivyo.*

**22. NARRATOR:**

Kulingana na Idrissa Konaté, wanaume hawa wanaamini ikiwa mume wa kwanza, wa pili au hata wa tatu alifariki, basi mume atakayefuta naye pia atafariki dunia. Mwanamke akikataliwa na wanaume kwa kuwa yeye ni mjane, basi hiyo ni aina fulani ya ubaguzi. Hata mwanamume aliyefiliwa na mke akikataliwa na wanawake ni ubaguzi pia.

Kuna wanaume wanaowachukulia wajane kuwa wanawake wa kumaliza tamaa zao za kimwili. Mtaalamu wa elimu-jamii Aliou Fofana, anayefanya utafiti kuhusu familia, anatutolea mfano wa mwanamke mjane



aliyebughudhiwa kijinsia na wanaume fulani aliokuwa ameenda kuwataka msaada.

**29. CLIP ALIOU FOFANA (French)**

*Alitegemea sana wahisani ili apate cha kuwalisha watoto wake. Baadhi ya watu walimsaidia kwa dhiti; ilhali wengine walitumia fursa hiyo kumbughudhi.*

**30. NARRATOR:**

Kisa cha Aminata kinathibitisha ukweli wa mambo. “Wanaume hupenda kuwa na uhusiano na wajane vijana, ” anasema. “Ukiwaruhusu, wataishia kukutumia vibaya.”

Barani Afrika, wajane hawalindwi kijamii. Kuna mashirika machache sana yaliyoundwa kushughulikia wajane. Hakuna sheria inayowalinda.

Zaidi ya hayo, wajane mara nyingi hutelekezwa na jamaa zao wa karibu.

Uhusiano kati ya Aminata na mashemeji zake uliharibika zaidi kwani baada ya kifo cha mumewe, alihama bila kuwajulisha jamaa za mumewe. Wakati mume wake alipokuwa hai walikuwa wakiishi wote kwenye nyumba ya wakwe zake.

**31. CLIP AMINATA (French)**

*Kabla hajaoa alikuwa akiwasaidia jamaa zake. Lakini alipooa asingeweza kuwasaidia tena kwa sababu alihitajika pia kutunza aila yake, watoto pamoja na mimi mkewe. Jamaa zake hawakupendezwa na jambo hilo wakawa wanadai kwamba alikuwa akinipa kila kitu. Hata kabla ya hapo hawakuwa wakinipenda. Alipokuwa hai walijifanya kwamba walikuwa wakinipenda, lakini*

*alipoaga dunia wakajitoa kimasomaso: walikuwa wamenikubali tu kwa sababu ya ndugu yao. Kwa hivyo nikaamua kujisimamia.*

**32. NARRATOR:**

Katika hali kama hii, suala la urithi ni tete. Wajane mara nyingi hupokonywa haki zao- kwa kuwa hawajui jinsi ya kuzitetea haki hizo. Aminata naye pia yumo.

**33. CLIP AMINATA (French):**

*Naam, aliwachia wanawe vitu vichache. Lakini kuna vitu vingine alivyoviacha ambavyo ilitubidi tugawanye, yaani: kati yangu na jamaa zake. Hadi leo sijapata haki yangu, kwa kuwa ndugu zake na mama yake walikataa kuidhinisha.*

**34. NARRATOR:**

Utaratibu wa kiserikali na kisheria kupata sehemu yake ya urithi, ni mrefu na unatatiza- kwa kuwa kwanza ada za mawakili ziko juu na wajane wengi hawana uwezo wa kuzilipa ada hizo. Mara nyingi hawana budi ila kuacha kutetea haki zao.

**35. MUSIC: Senegalese rap**

**36. NARRATOR:**

Bado kungali na mambo mengi ya kufanywa kumaliza ubaguzi huu wa wajane. Lakini Aminata anataka kusaidia kuendeleza harakati za utetezi.

**Learning by Ear 2012 – Minorities  
Episode 09 - Widows**

Anatumai kuwa siku za usoni atanzisha chama cha wajane vijana nchini Senegal. “Shirika hilo,” anasema, “litakuwa kimbilio la kila mjane humu nchini.”

**OUTRO:**

Na mpaka hapo ndipo tunapofikia mwisho wa sehemu hii ya kipindi cha **Noa Bongo Jenga Maisha Yako**. Taarifa hii iliandaliwa na Babou Diallo, na ni sehemu ya kipindi chetu kinachoshughulikia ‘**Kuzingatia maslahi ya jamii za walio wachache**’. Ukitaka kuisikiliza sehemu hii, au sehemu nyingine ya kipindi hiki, fungua wavuti wetu [dw.de/lbe](http://dw.de/lbe). Tunakushuru kwa kutusikiliza-  
Kwaheri!